


EPISCOPAL CHURCH of the
HEAVENLY REST

God's Love. For All.

Tatu Mbele Ya Kuja
Jumapili, Novemba 9, 2025
Saa 1:00 jioni



Third Sunday Before Advent
Morning Prayer in Swahili
Sunday, November 9, 2025
1:00 in the afternoon

Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe, naye alitupa sisi utumishi wa upatanisho.

WIMBO WA KUINGILIA

Wote kusimama

WITO WA KUABUDU

Tumekusanyika pamoja kama jamaa ya Mungu mbele ya Baba yetu, tukivutwa na Roho yake, kusifu Jina lake, kusikia na kupokea Neno lake takatifu. kumwomba usamehe kwa zambi zetu, kuombea mahitaji yetu na ya dunia, kufurahi katika mapendo yake, na kutumwa katika salama yake.

MWALIKO

Ee Bwana, ufungue midomo yetu.

Na kinywa chetu kitaonyesha sifa yako.

Katika Nyakati Nyingine:

Bwana rehema zako ni mpya kila asubui.

Uaminifu wako ni mukubwa!

Tangu mapambazuko hata mangaribi.

Jina la Bwana lisifiwe.

Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine.

WIMBO

KUUNGAMA DHAMBI

Muhudumu aseme:

Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu.

Tukikiri zambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, hata atatuondolea zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote.

1 Yoane 1:8-9

Muhudumu aseme:

Tukiri zambi zetu kwa Mungu Mwenyezi.

Wote wapige magoti na kusema

Mungu Mwenyezi, Baba yetu ya mbinguni, tumekosea wewe, na tumekosea jirani zetu, kwa mawazo yetu, na kwa maneno yetu, na kwa matendo yetu, na kwa maovu tuliyoyatenda, na kwa mema tusiyoyatenda, kosa letu wenyewe. Sisi tunatubu kabisa. Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo, utusamehe yote yaliyopita; utuwezeshe tangu leo kukutumikia, katika upya wa uzima. Kwa utukufu wa Jina lako. Amina.

Muhudumu au mutu mwingine asiye Kasisi, akipiga magoti atumie ombi hili.

Ee Mungu, mwenye rehema, tunakusihi, utupe sisi, watu wako waaminifu, usamehe na salama, ili tusafishwe zambi zetu zote, na tukutumikie na nia tulivu; kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Amina.

Zaburi ya Siku isomwe au iimbwe.

ZABURI 17:1-9

1 Ee Bwana, usikie haki, ukisikilize kilio changu, Utege sikio lako kwa maombi yangu, Yasiyotoka katika midomo ya hila.

2 Hukumu yangu na itoke kwako, Macho yako na yatazame mambo ya adili.

3 Umenijaribu moyo wangu, umenijilia usiku, Umenihakikisha usione neno; Nimenuia kinywa changu kisikose,

4 Mintarafu matendo ya wanadamu; Kwa neno la midomo yako Nimejiepusha na njia za wenye jeuri.

5 Nyayo zangu zimeshikamana na njia zako, Hatua zangu hazikuondoshwa.

OPENING SENTENCE

2 Corinthians 5:19

God was in Christ, reconciling the world to himself, and gave to us the ministry of reconciliation.

PROCESSIONAL HYMN

Stand for the Procession

CALL TO WORSHIP

We are gathered together as God's family before our Father, drawn by his Spirit, to praise his Name, to hear and receive his holy Word. to ask him to forgive us for our sins, to pray for our needs and the needs of the world, to rejoice in his love, and to be sent to his safety.

INVITATORY

O Lord, open our lips.

And our mouth shall proclaim your praise.

At Other Times:

Lord, your mercy is new every morning.

Great is your faithfulness!

From dawn to dusk.

May the name of the Lord be praised.

A song from the Bible or another song is sung.

HYMN

CONFESSION OF SIN

The Minister should say:

If we say that we have no sin, we deceive ourselves, and the truth is not in us. If we confess our sins, he who is faithful and just will forgive us our sins and cleanse us from all unrighteousness.

1 John 1:8-9

The Minister should say:

Let us confess our sins to God Almighty.

All should kneel and say:

Almighty God, our heavenly Father, we have sinned against you and against our neighbors, in thought and word and deed, in the evil we have done and in the good we have not done, through our own deliberate fault. We are truly sorry, and repent of all our sins. For the sake of your Son Jesus Christ, who died for us, forgive us all that is past; and grant that we may serve you in newness of life to the glory of your name. Amen.

A minister or other person who is not a priest, kneeling should use this request:

Grant, we ask you, merciful Lord, to your faithful people pardon and peace, that they may be cleansed from all their sins, and serve you with a quiet mind, through Jesus Christ our Lord.
Amen.

The Psalm of the Day should be read or sung.

PSALM 17:1-9

1 Hear my plea of innocence, O Lord; give heed to my cry; listen to my prayer, which does not come from lying lips.

2 Let my vindication come forth from your presence; let your eyes be fixed on justice.

3 Weigh my heart, summon me by night, melt me down; you will find no impurity in me.

4 I give no offense with my mouth as others do; I have heeded the words of your lips.

5 My footsteps hold fast to the ways of your law; in your paths my feet shall not stumble.

6 I call upon you, O God, for you will answer me; incline your ear to me and hear my words.

7 Show me your marvelous loving-kindness, O Savior of those who take refuge at your right

6 Ee Mungu, nimekuita kwa maana utaitika, Utege sikio lako ulisikie neno langu.
7 Dhihirisha fadhili zako za ajabu Wewe uwaokoaye wanaokukimbilia; Kwa mkono wako wa kuume Uwaokoe nao wanaowaondokea.
8 Unilinde kama mboni ya jicho, Unifiche chini ya uvuli wa mbawa zako;
9 Wasinione wasio haki wanaonionea, Adui za roho yangu wanaonizunguka.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:
kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa, hata milele na milele. Amina.

WIMBO

Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO LA KALE kisomwe.

SOMO LA KWANZA

Yobu 19:23-27a

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Kitabu cha Yobu.

Laiti maneno yangu yangeandikwa sasa! Laiti yangeandikwa kitabuni! Yakachorwa katika mwamba milele, Kwa kalamu ya chuma na risasi. Lakini mimi najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, Lakini, pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu; Nami nitamwona mimi nafsi yangu, Na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine.

Hilo ndilo Neno la Bwana.
Asante kwa Mungu.

WIMBO

Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO JIPIYA kisomwe.

SOMO LA PILI

2 Watesalonika 2:1-5, 13-17

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Barua kwa Watesalonika.

Basi, ndugu, tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake, kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu, wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. Je! Hamkumbuki ya kuwa wakati nilipokuwapo pamoja nanyi naliwaambieni hayo?

Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana, kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli; aliyowaitia ninyi kwa injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo. Basi, ndugu, simameni imara, mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu. Na Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe, na Mungu Baba yetu, aliyetupenda akatupa faraja ya milele na tumaini jema, katika neema, awafariji mioyo yenu, na kuwafanya imara katika kila neno na tendo jema.

Hilo ndilo Neno la Bwana.
Asante kwa Mungu.

WIMBO

hand from those who rise up against them.

8 Keep me as the apple of your eye; hide me under the shadow of your wings,

9 From the wicked who assault me, from my deadly enemies who surround me.

Glory be to the Father, and to the Son, and to the Holy Spirit:

As it was in the beginning, is now, and ever shall be, world without end. Amen.

HYMN

All Sit. A passage from the OLD TESTAMENT should be read.

FIRST READING

Job 19:23-27a

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Book of Job.

“O that my words were written down! O that they were inscribed in a book! O that with an iron pen and with lead they were engraved on a rock forever! For I know that my Redeemer lives, and that at the last he will stand upon the earth; and after my skin has been thus destroyed, then in my flesh I shall see God, whom I shall see on my side, and my eyes shall behold, and not another.”

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

All Sit. A passage from the NEW TESTAMENT should be read.

SECOND READING

2 Thessalonians 2:1-5, 13-17

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Second Letter to the Thessalonians.

As to the coming of our Lord Jesus Christ and our being gathered together to him, we beg you, brothers and sisters, not to be quickly shaken in mind or alarmed, either by spirit or by word or by letter, as though from us, to the effect that the day of the Lord is already here. Let no one deceive you in any way; for that day will not come unless the rebellion comes first and the lawless one is revealed, the one destined for destruction. He opposes and exalts himself above every so-called god or object of worship, so that he takes his seat in the temple of God, declaring himself to be God. Do you not remember that I told you these things when I was still with you?

But we must always give thanks to God for you, brothers and sisters beloved by the Lord, because God chose you as the first fruits for salvation through sanctification by the Spirit and through belief in the truth. For this purpose he called you through our proclamation of the good news, so that you may obtain the glory of our Lord Jesus Christ. So then, brothers and sisters, stand firm and hold fast to the traditions that you were taught by us, either by word of mouth or by our letter. Now may our Lord Jesus Christ himself and God our Father, who loved us and through grace gave us eternal comfort and good hope, comfort your hearts and strengthen them in every good work and word.

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Injili ya Luka Mutakatifu.

Kisha baadhi ya Masadukayo wakamwendea, wale wasemao ya kwamba hakuna ufufuo, wakamwuliza, wakisema, Mwalimu, Musa alituandikia ya kuwa, mtu akifiwa na ndugu yake mwenye mke, lakini hana mtoto na amtwe huyu mke, ampatie ndugu yake mzao. Basi, kulikuwa na ndugu saba. Wa kwanza alioa mke, akafa hana mtoto; na wa pili [akamtwea yule mke, akafa hana mtoto;] hata wa tatu akamwoa, na kadhalika wote saba, wakafa, wasiache watoto. Mwisho akafa yule mke naye. Basi, katika ufufuo atakuwa mke wa yupi? Maana aliolewa na wote saba. Yesu akawaambia, Wana wa ulimwengu huu huoa na kuolewa; lakini, wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi; wala hawawezi kufa tena; kwa sababu huwa sawasawa na malaika, nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo. Lakini, ya kuwa wafu hufufuliwa, hata na Musa alionyesha katika sura ya Kijiti, hapo alipomtaja Bwana kuwa ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Naye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai; kwa kuwa wote huishi kwake.

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO WA INJILI

KUHUBIRI

Bikole Mulanda, *Waziri wa Usharika wa Kiswahili*

IMANI YA MITUME

Watu wasimame kuhakikisha IMANI YA MITUME

Ninamwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia; Na Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu, aliyetwea mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu, akazaliwa na Bikira Maria. Akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimuni mwa wafu, akafufuka katika wafu siku ya tatu, akapanda mbinguni, anakaa kwa mukono wa kuume wa Mungu, Baba Mwenyezi, ndipo atakuja tena kuhukumu wazima na wafu. Ninamwamini Roho Mutakatifu, Kanisa katolika takatifu, ushirika wa watakatifu, on-doleo la zambi, ufufuko wa mwili, na uzima wa milele. Amina.

MAOMBI

Kupiga magoti

Muhudumu Bwana utuhurumie.

Wote **Kristo utuhurumie.**

Muhudumu Bwana utuhurumie.

SALA YA BWANA

Wote

Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, duniani kama mbinguni. Utupe leo chakula chetu cha kila siku; utusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe waliotukosea. Usitulete katika majaribu, lakini utuokoe katika uovu. Kwani kwako ufalme, uwezo na utukufu, milele na milele, Amina.

Muhudumu Ee Bwana utuonyeshe rehema yako;

Wote **Utupe sisi wokovu wako.**

Muhudumu Ee Bwana uwabariki watawala wetu;

Wote **Utusikie kwa rehema yako tukikuomba.**

Muhudumu Uwavike haki wahudumu wako;

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Gospel of St. Luke.

Some Sadducees, those who say there is no resurrection, came to Jesus and asked him a question, "Teacher, Moses wrote for us that if a man's brother dies, leaving a wife but no children, the man shall marry the widow and raise up children for his brother. Now there were seven brothers; the first married, and died childless; then the second and the third married her, and so in the same way all seven died childless. Finally the woman also died. In the resurrection, therefore, whose wife will the woman be? For the seven had married her." Jesus said to them, "Those who belong to this age marry and are given in marriage; but those who are considered worthy of a place in that age and in the resurrection from the dead neither marry nor are given in marriage. Indeed they cannot die anymore, because they are like angels and are children of God, being children of the resurrection. And the fact that the dead are raised Moses himself showed, in the story about the bush, where he speaks of the Lord as the God of Abraham, the God of Isaac, and the God of Jacob. Now he is God not of the dead, but of the living; for to him all of them are alive."

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN OF THE GOSPEL

SERMON

Bikole Mulanda, *Swahili Minister*

THE APOSTLES' CREED

All People should stand and say the APOSTLES' CREED:

I believe in God, the Father almighty, creator of heaven and earth; I believe in Jesus Christ, his only Son, our Lord. He was conceived by the power of the Holy Spirit and born of the Virgin Mary. He suffered under Pontius Pilate, was crucified, died, and was buried. He descended to the dead. On the third day he rose again. He ascended into heaven, and is seated at the right hand of the Father. He will come again to judge the living and the dead. I believe in the Holy Spirit, the holy catholic Church, the communion of saints, the forgiveness of sins the resurrection of the body, and the life everlasting. Amen.

THE PRAYERS

All that are able to should kneel:

Minister Lord, have mercy upon us.

All **Christ, have mercy upon us.**

Minister Lord, have mercy upon us.

THE LORD'S PRAYER

All pray.

Our Father in heaven, hallowed be your Name, your kingdom come, your will be done, on earth as in heaven. Give us today our daily bread. Forgive us our sins as we forgive those who sin against us. Save us from the time of trial, and deliver us from evil. For the kingdom, the power, and the glory are yours, now and for ever. Amen.

Minister Show us your mercy, O Lord;

All **And grant us your salvation.**

Minister O Lord, save the State;

All **And mercifully hear us when we call upon you.**

Minister Endue your ministers with righteousness;

Wote **Uwafurahishe wachaguliwa wako.**
Muhudumu Ee Bwana uwaokoe watu wako;
Wote **Uubariki uriti wako.**
Muhudumu Ee Bwana utupe salama kwa siku zetu;
Wote **Na utukufu wako uwe popote duniani.**
Muhudumu Ee Mungu, utusafishe mioyo yetu;
Wote **Na ututegemeze na Roho yako Mutakatifu.**

SALA YA SIKU

Baba Mwenyezi, mapenzi yako ni kurudisha vyote kwa utaratibu na umoja katika Mwana wako, Mufalme wa wote, utawale mioyo na nia za wenye mamlaka, na ulete jamaa za mataifa zilizotengana kwa uharibifu wa zambi, kuwa chini ya utawala wake wa haki na upole: anayeishi na kutawala pamoja nawe na Roho Mutakatifu, Mungu mumoja, sasa hata milele. **Amina.**

SALA KWA SALAMA

Baba Mungu, uliye mkuu wa salama na mupenda wa upatano, kukujua wewe ni uzima wa milele, kukutumikia wewe ni uhuru wa kweli. Utulinde sisi watumishi wako katika mashambulio yote ya adui zetu; ili sisi tukitumainia ulinzi wako, tusiogope nguvu ya adui wa wote; kwa uwezo wa Yesu Kristo, Bwana wetu. **Amina.**

SALA KWA NEEMA

Muhudumu na watu wanaweza kusema pamoja.

Ee Bwana, Baba yetu ya mbinguni, Mungu Mwenyezi unayeishi milele, uliyetusaidia tuione siku hii salama; utulinde leo kwa uwezo wako mkuu, tusianguke katika zambi, wala tusiingie katika hatari ya yote, lakini matendo yetu yote yaongozwe nawe, ili tuyatende siku zote yaliyo ya haki mbele yako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

MAOMBI YA KANISA

Muhudumu Tuombee Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

Mwombezi huomba kwa ajili ya mahitaji ya kanisa na ya ulimwengu pasipo kuona.

Muombezi anamaliza sala kwa maneno haya:

Na tunalisifu jina lako takatifu kwa watumishi wako wote wanaotoka katika uzima huu, wanaokuamini na wanaokuogopa. Tunakusihi utupe neema tufuate desturi zao nzuri, tukutane nao katika ufalme wako wa mbinguni. Utupe sisi hivi, Ee Bwana, kama tunavyoviomba kwa Yesu Kristo Mwana wako, Mwokozi wetu. **Amina.**

Maombi mengine yanaweza kusemwa.

MATANGAZO NA SADAKA

Wimbo na kupokea sadaka.

NEEMA

Watu Wote.

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mutakatifu, ukae nasi sote, milele na milele. Amina.

WIMBO YA KUTOKA

All **And make you chosen people joyful.**
Minister O Lord, save your people;
All **And bless your inheritance.**
Minister Give peace in our time, O Lord.
All **May your glory be everywhere in the world .**
Minister O God, make clean our hearts within us;
All **And take not your Holy Spirit from us.**

THE COLLECT OF THE DAY

Almighty Father, it is your will to restore all things to order and unity in your Son, the King of all, to rule the hearts and minds of those in authority, and to bring the families of nations separated by the destruction of sin, under his just and gentle rule: who lives and reigns with you and the Holy Spirit, one God, now and forever. **Amen.**

THE COLLECT FOR PEACE

O God, who art the author of peace and lover of concord, in knowledge of whom standeth our eternal life, whose service is perfect freedom: Defend us, thy humble servants, in all assaults of our enemies; that we, surely trusting in thy defense, may not fear the power of any adversaries; through the might of Jesus Christ our Lord. **Amen.**

THE COLLECT FOR GRACE

The Minister and the people say this prayer together.

O Lord, our heavenly Father, almighty and everlasting God, who has safely brought us to the beginning of this day; defend us in the same with your mighty power; and grant that this day we fall into no sin, neither run into any kind of danger, but that all our doings may be ordered by your governance, to do always that is righteous in your sight; through Jesus Christ our Lord. Amen.

PRAYERS OF THE CHURCH

Minister Let us pray for the Church and the world and let us thank God for all his goodness.

The intercessor prays for the needs of the church and the world extemporaneously.

The intercessor ends the prayer with these words:

And we praise your holy name for all your servants who have departed this life, who believe in you and who fear you. We ask you to give us the grace to follow their good example, to meet them in your heavenly kingdom. Grant this, O Lord, as we ask for it from Jesus Christ your Son, our Savior. **Amina.**

Other prayers may be said.

ANNOUNCEMENTS AND OFFERING

A song is sung during the offering.

THE GRACE

All Say

The grace of our Lord Jesus Christ, and the love of God, and the fellowship of the Holy Spirit, be with us all evermore. Amen.

RECESSIONAL HYMN

WAHUDUMU WA LITURUJIA

Muhubiri/Preacher - Bikole Mulanda, Swahili Minister

Kwaya/Choir - Aleluya Kwaya

Washemasi/Greeters & Ushers - Baya Lushiawe, Mkyombwe



602 Meander Street Phone: (325) 677-2091
Abilene, Texas 79602 Email: info@heavenlyrestabilene.org
Website: heavenlyrestabilene.org Social media: [@heavenlyrestabilene](https://www.facebook.com/heavenlyrestabilene)

CLERGY AND STAFF

The Reverend David F. Romanik, <i>Rector</i>	Carol Ann Weston, <i>Director of Children & Family Ministries</i>
The Reverend Ashley Powers, <i>Associate Rector</i>	Thomas Pavlechko, <i>Organist and Director of Music</i>
The Reverend Amanda Watson, <i>Assistant Rector for Community Life</i>	Elizabeth Knauer, <i>Music Assistant, Choristers</i>
The Reverend Karen Boyd, <i>Assisting Priest</i>	Laura Dickson, <i>Music Assistant, Children's Choir</i>
The Reverend Dr. Doug Thomas, <i>Priest in Residence</i>	Jen Rogers, <i>Director of Communications and Stewardship</i>
The Reverend Dr. Russell Dickerson, <i>Deacon</i>	Lydia Hurt, <i>Parish Manager</i>
The Reverend Joe Biles, <i>Deacon and Pastoral Assistant</i>	Brenda Fisher, <i>Parish Accountant</i>
Bikole Mulanda, <i>Swahili Minister</i>	Robert Becerra, <i>Sexton</i>
Luke Teten, <i>Verger</i>	Dorothy Guerra, <i>Housekeeper</i>
	Anne Jones, <i>Nursery Manager</i>

VESTRY AND APPOINTED OFFICERS

Kate Haney, *Senior Warden*; Harry Hurt, *Junior Warden*; Sharon Lawler, *Secretary*; David Christianson, Michael Christie, Dru Hall, Diane Stearns, Kimberly Brumley, Jay Hardaway, Norene Mansell, John Nichols, Mary Reyes, Elizabeth Niblo Wallace, *Chancellor*; and Sam Cutbirth, *Treasurer*